

Title	Utofauti wa Kilahaja wa Kiswahili : Kutokana na Data Zilizokusanywa Kisiwani Unguja
Author(s)	Takemura, Keiko; Miyazaki, Kumiko
Citation	スワヒリ&アフリカ研究. 2019, 30, p. 67-80
Version Type	VoR
URL	https://doi.org/10.18910/72918
rights	
Note	

Osaka University Knowledge Archive : OUKA

<https://ir.library.osaka-u.ac.jp/>

Osaka University

Utofauti wa Kilahaja wa Kiswahili - Kutokana na Data Zilizokusanywa Kisiwani Unguja -¹⁾

TAKEMURA Keiko na MIYAZAKI Kumiko

O. Utangulizi

Makala hii inajaribu kuonyesha utofauti wa kilahaja wa Kiswahili hasa unaoonekana kimsamiati na kimofosintaksia kisiwani Unguja, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Kiswahili kinasemwa katika sehemu za pwani na visiwani huko Afrika ya Mashariki, na takriban lahaja 24 zimerekodiwa katika makala na kazi zilizoandikwa siku za nyuma. Kisiwani Unguja, inasemekana kwamba lahaja kuu tatu zinatumiwa; lahaja ya Kaskazini, lahaja ya Kusini na lahaja ya Unguja-Mjini.

Kama tunavyojua, Kiswahili kimesanifishwa kuwa “Kiswahili Sanifu” mwaka 1930 kwa kuongozwa na Kamati ya Lugha (Kiswahili) ya Makoloni iliyoanzishwa na Serikali ya Kikoloni ya Uingereza. Kiswahili Sanifu kinatumika rasmi nchini Tanzania kwa mfano katika elimu rasmi.

Kiunguja-Mjini kinasemekana kama ndio msingi wa Kiswahili Sanifu, lakini kusema la kweli Kiswahili Sanifu na Kiunguja-Mjini si Kiswahili kimoja. Na tena, kama tulivyotaja juu, ingawa kisiwani Unguja inasemekana kuwa zipo lahaja kuu tatu, lakini data mpya zilizokusanywa katika vijiji kadhaa vya Unguja zinatunyesha kwamba utafiti wa dhati hasa na uchambuzi zaidi wa lahaja za Unguja unahitaji kufanyika. Isitoshe, kumekuwa na majadiliano machache tu juu ya uhusiano baina ya Kiswahili Sanifu na lahaja nyingine, na vilevile inaonekana kuwa majadiliano juu ya utofauti wenyewe wa lahaja hizo hayatoshelezi.

Katika makala hii tutajaribu kuripoti juu ya tofauti za kimatumizi za lahaja za kisiwani Unguja, yaani Kiunguja-Mjini, na lahaja za sehemu za Kaskazini; Kichaani, Kikibeni, Kitumbatu-Gomani, Kinungwi na Kimatemwe, na lahaja za sehemu za Kusini; Kijambiani, Kipaje na Kimakunduchi, hasa kwa kuzingatia tofauti za kimsamiati. Halafu tutaonyesha pia utofauti wa kisarufi wa lahaja kadhaa, yaani lahaja za sehemu za Kaskazini; Kichaani, Kikibeni, Kitumbatu-Gomani, Kinungwi, na lahaja za sehemu za Kusini; Kijambiani na Kipaje. Tutaonyesha hasa tofauti za Njeo/Hali, Sentensi zinazotumia Kopyula, Kauli zinazotumia Viambishi-Rejeshi, na Dhamira Amri. Kutokana na data tulizokusanya, tutajaribu kufafanua utofauti wa lahaja na lahaja kwa upande mmoja, na tofauti baina ya lahaja hizo na Kiunguja-Mjini²⁾ kwa upande mwingine.

¹⁾ Makala hii asili yake ni makala ya Kiingereza iliyotolewa katika Mkutano wa Tisa wa Kimataifa wa Isimu ya Lugha ya Afrika (yaani WOCAL 9) uliofanyika Rabat, Morocco kuanzia tarehe 24 mpaka 28 mwezi wa 8 mwaka 2018. Mada yake ilikuwa “Towards a new approach to ‘Viswahili’ in Zanzibar”. Mara hii mwandishi mmojawapo wa makala ya Kiingereza yaani mimi TAKEMURA Keiko nimeitafsiri na kuiongezea maelezo kadhaa kwa Kiswahili.

²⁾ Data zote zinazotumiwa katika makala hii zilikusanywa na TAKEMURA Keiko na MIYAZAKI Kumiko katika tafiti kadhaa. Tafiti zote ziliendeshwa na bajeti rasmi ya Wizara ya Elimu na Sayansi ya Japani, inayoitwa “Grant-in-Aid for Scientific Reseach (KAKENHI)”. Jina la mradi wa kwanza ni: Kuunda Eneo la Kiutamaduni na Miundo ya Kikabila Inayozalishwa na Lugha ya Mawasiliano ya Afrika ya Mashariki (Kiongozi: Prof. MIYAMOTO Masaoki, Muda wa Mradi: 1996-1998). Jina la mradi wa pili ni: Utafiti wa Maoni ya Kijinsia na Historia ya Kimaisha katika Pwani ya Afrika ya Mashariki - Kutokana na ‘Masimulizi’ ya Wanawake - (Kiongozi: TAKEMURA Keiko, Muda wa Mradi: 2009-2011). Jina la mradi wa tatu ni: Utafiti wa Kuhifadhia Lahaja Kadhaa za Kiswahili katika Afrika ya Mashariki (Kiongozi: TAKEMURA Keiko, Muda wa Mradi: 2011-2013). Jina la mradi wa nne ni: Utafiti wa Kuhifadhia Lahaja Kadhaa za Kiswahili Visiwani Zanzibar - Hasa juu ya Tofauti za Kisarufi na Kimsamiati - (Kiongozi: TAKEMURA Keiko, Muda wa Mradi: 2016-2018).

1. Utofauti wa Kimsamiati

Kwanza tutaangalia utofauti wa kimsamiati. Mifano ya (1) inatuonyesha tofauti za kimsamiati baina ya Kiunguja-Mjini na lahaja za sehemu mbalimbali. Data zinasema wazi kwamba hata msamiati wa lahaja za Unguja pamoja na Kiunguja-Mjini unaotumika kila siku unatofautiana na msamiati unaoandikwa katika kamusi au unaotumika bara. Mfano wa (1)a ni neno lenye maana ya ‘fleas’: Kwa Kiswahili Sanifu umoja wake ni *funza* ngeli ya 9, na wingi wake pia *funza* ngeli ya 10. Kwa lahaja za Unguja, umoja wake ni *chepu* ngeli ya 9, na wingi wake pia *chepu* ngeli ya 10. Wahojiwa wengine walijibu kama umoja wake ni *chepu* ngeli ya 9, lakini wingi wake *machepu* ngeli ya 6.

Mfano (1)b ni neno lenye maana ya ‘tomato’: Kwa Kiswahili Sanifu umoja wake ni *nyanya* ngeli ya 9, na wingi wake ni sawasawa na umoja, *nyanya*, ngeli ya 10. Kwa Kiunguja-Mjini na Kichaani, umoja wake ni *t’ungule* ngeli ya 9, na wingi wake ni *t’ungule* ngeli ya 10; sauti /t/ inatamkwa na mpumuo. Halafu kwa Kijambiani na Kipaje, umoja wake ni *tungule* ngeli ya 9, na wingi wake ni *tungule* ngeli ya 10. Na sauti ya /t/ ya lahaja hizi mbili hazitamkwi na mpumuo, yaani /t/ ya kawaida tu. Kwa maneno mengine tunaweza kusema kuwa lahaja hizi za Unguja zinatumia msamiati tofauti kabisa na ule wa Kiswahili Sanifu. Kisiwani Unguja neno *nyanya* linamaanisha matunda ya mmea mwingine kabisa, matunda hayo bila shaka yanaonekana kama ‘small tomato’ lakini yana ladha chungu (bitter) sana.

(1)

a. ‘flea’

funza/funza	[Kiswahili Sanifu]
chepu/chepu au chepu/machepu	[Kiunguja-Mjini]
kepu/kepu au kepu/makepu	[Kichaani / Kijambiani / Kipaje]

b. ‘tomato’

nyanya/nyanya	[Kiswahili Sanifu]
t’ungule/t’ungule	[Kiunguja-Mjini / Kichaani]
tungule/tungule	[Kijambiani / Kipaje]

Data zilizomo katika mifano ya (2) zinaonyesha tofauti baina ya Kiunguja-Mjini na lahaja nyingine. Mfano (2)a ni neno lenye maana ya ‘spider’; ingawa msamiati wa Kiunguja-Mjini ni sawasawa na wa Kiswahili Sanifu, lakini tukiangalia umbo lake la wingi, inafahamika kuwa ni sawasawa na msamiati wa lahaja nyingine. Kwa upande mwingine, mfano (2)b, neno lenye maana ya ‘mango’; unaonyesha aina nyingine ya utofauti. Wasemaji wengine wa Kiunguja-Mjini wanatumia msamiati sawasawa na wa Kiswahili Sanifu, yaani umoja wake ni *embe* ngeli ya 5 na wingi wake ni *maembe* ngeli ya 6, lakini wengine wanatumia neno moja kwa umoja na wingi wake kama wanavyotumia wasemaji wa lahaja nyingine. Hii inatuonyesha kwamba kuna uwezekano wa kutokea mabadiliko ya ngeli, yaani wakati Kiswahili kiliposanifishwa msamiati wenye maana ya ‘fruit’ (*tunda/matunda*) ulibadilishwa ngeli yake kutoka ngeli ya 9/10 kwenda ngeli ya 5/6. Vilevile inasemekana kuwa baadhi ya msamiati wenye maana ya ‘fruit’ bado umebaki katika ngeli ya 9/10 katika lahaja nyingine kwa kufuata mfumo wa kiasili wa ngeli.

(2)

a. 'spider'

buibui/buibui	[Kiswahili Sanifu]
buibui/mabuibui	[Kiunguja-Mjini]
bui/mabui	[Kichaani / Kijambiani / Kipaje]

b. 'mango'

embe/maembe	[Kiswahili Sanifu / Kiunguja-mjini]
embe/embe	[Kiunguja-mjini / Kijambiani / Kipaje]
iembe/iembe	[Kinungwi / Kimatemwe]
yembe/yembe	[Kichaani / Kikibeni]

Na tena, kama mfano (3) unavyoonyesha, kuna utofauti mkubwa mno kati ya lahaja na lahaja. Mfano wa (3)a ni neno lenye maana ya 'butterfly'. Kwa Kiswahili Sanifu umoja wake ni *kipepeo* ngeli ya 7, wingi wake ni *vipepeo* ngeli ya 8. Jozi kama hii ya umoja/wingi inaonekana katika Kiunguja-Mjini na Kijambiani pia. Lakini kwa Kichaani, umoja wake ni *bangawi* ngeli ya 9, na wingi wake ni *bangawi* ngeli ya 10 au *mabangawi* ngeli ya 6. Vilevile, kwa Kipaje na Kimakunduchi, umoja wake ni *kitunguja* ngeli ya 7, na wingi wake ni *vitunguja* ngeli ya 8. Kwa hivyo tulipata msamiati tofauti katika lahaja hizi.

(3)

a. 'butterfly'

kipepo/vipepeo	[Kiswahili Sanifu / Kiunguja-Mjini / Kijambiani]
bangawi/bangawi au mabangawi	[Kichaani]
kitunguja/vitunguja	[Kipaje / Kimakunduchi]

2. Utofauti wa Kisarufi

Katika sehemu hii tunatazama tofauti kadhaa za kisarufi. Sehemu ya 2.1 tunatazama utofauti wa njeo/hali, sehemu ya 2.2 tunatazama utofauti wa sentensi zinazotumia kopyula, sehemu ya 2.3 tunatazama utofauti wa kauli zenye viambishi-rejeshi, na sehemu ya 2.4 tunatazama utofauti wa dhamira amri.

2.1. Njeo / Hali

Mifano ya sentensi zenye njeo iliyopo: Mfano wa (4)a unaonyesha Kiswahili Sanifu na Kiunguja-Mjini, (4)b ni Kichaani, Kikibeni, Kinungwi, Kijambiani, na (4)c ni Kitumbatu-Gomani. Kama tunavyoona, kuna tofauti ndogondogo kama kuwepo au kutokuwepo kiambishi-kiima, au kiambishi-njeo kuwa *-na-* ama *-a-*. Lakini kwa vyovyote vile, inawezekana kusema hakuna utofauti mkubwa katika sentensi zenye njeo iliyopo. Tuongeze kutaja kwamba inaonekana wasemaji wengine wa Kitumbatu-Gomani hasa vijana wanasema zaidi kama (4)b kuliko (4)c.

(4) 'I study Swahili.'

- a. Ni-na-som-a Ki-swahili. [Kiswahili Sanifu / Kiunguja-Mjini]
SM1sg-Prs-study-FV cl7-Swahili
- b. ϕ-na-som-a Ki-swahili. [Kichaani / Kikibeni / Kinungwi / Kijambiani / Kipaje]
SM1sg-Prs-study-FV cl7-Swahili
- c. Ni-a-som-a (> Nyasoma) Ki-swahili. [Kitumbatu-Gomani]
SM1sg-Prs-study-FV cl7-Swahili

Mfano wa (5)a unaonyesha sentensi ya kukanusha yenye njeo iliyopo ya Kiswahili Sanifu na Kiunguja-Mjini, na (5)b ni ya Kichaani, Kitumbatu-Gomani, Kikibeni, Kinungwi, Kipaje na Kijambiani. Kama tunavyoona hapa, tofauti kuu ni kwamba hakuna kiambishi-njeo katika sentensi ya Kiswahili Sanifu na Kiunguja-Mjini bali kiambishi hicho kipo katika lahaja nyingine zote.

(5) 'I don't study Swahili.'

- a. si-som-i Ki-swahili. [Kiswahili Sanifu / Kiunguja-Mjini]
NegSM1sg-study-NegV cl7-Swahili
- b. si-na-som-a Ki-swahili. [Kichaani / Kitumbatu-Gomani / Kikibeni / Kinungwi / Kipaje /
NegSM1sg-Prs-study-NegV cl7-Swahili Kijambiani]

Mifano ya sentensi zenye njeo iliyopita: kuanzia (6)a mpaka (10)a inaonyesha sentensi za Kiswahili Sanifu na Kiunguja-Mjini. Mifano kuanzia (6)b mpaka (10)b inaonyesha za Kichaani, Kitumbatu-Gomani, Kikibeni, Kinungwi. Mifano ya (6)c na (7)c inaonyesha sentensi za Kijambiani na Kipaje tu kwa sababu lahaja hizi mbili kiambishi-kiini chake kinachomaanisha 'mimi' ni tofauti na kiambishi hicho katika lahaja nyingine. Mifano kuanzia (8)b mpaka (10)b inaonyesha sentensi za lahaja zote isipokuwa Kiswahili Sanifu na Kiunguja-Mjini.

Mfano wa (6) una maana ya 'I cut the meat'; mfano wa (7) una maana ya 'I did (it)'; mfano wa (8) una maana ya 'he/she wrote a/the letter'; mfano wa (9) una maana ya 'you saw him/her'; na mfano wa (10) una maana ya 'we pulled the rope'. Kama tunavyoona, katika sentensi za (6)a mpaka (10)a kiambishi-njeo ni *li*, lakini katika sentensi za (6)b mpaka (10)b pamoja na (6)c na (7)c, kiambishi hicho hakionekani. Badala yake, katika sentensi za (6)b mpaka (10)b na (6)c na (7)c, lazima kiwepo kiambishi-tamati chenye vokali sawa na vokali iliyopo mwishoni mwa mzizi wa kitenzi. Basi lahaja zote isipokuwa Kiswahili Sanifu na Kiunguja-Mjini hazina kiambishi-njeo cha njeo iliyopita bali zina kanuni ya kunakili vokali katika sentensi ya njeo iliyopita.

W. H. Whiteley (1955) aliandika pia katika makala yake kwamba lahaja inayosemwa sehemu za pwani baina ya Dar es Salaam na Tanga, yaani Kimtang'ata ina muundo sawasawa na muundo huo wa sentensi za njeo iliyopita za lahaja za Unguja kama mifano ya (6)b mpaka (10)b na (6)c na (7)c. Jambo hili linatusisimua sana kwani ingawa ndani ya kisiwa kimoja kuna utofauti wa kimsamiati na kisarufi kati ya lahaja na lahaja, kuna usawa wa kisarufi katika lahaja nyingine inayosemwa katika eneo la mbali la bara.

(6) 'I cut meat.'

- a. Ni-li-kat-a nyama. [Kiswahili Sanifu / Kiunguja-Mjini]
SM1sg-Pst-cut-FV cl9-meat
- b. Ni-kat-a nyama [Kichaani / Kijambiani / Kitumbatu-Gomani / Kikibeni / Kinungwi]
SM1sg-cut-PstF cl9-meat
- c. N-kat-a nyama [Kijambiani / Kipaje]
SM1sg-cut-PstF cl9-meat

(7) 'I did.'

- a. Ni-li-fany-a. [Kiswahili Sanifu / Kiunguja-Mjini]
SM1sg-Pst-do-FV
- b. Ni-tend-e. [Kichaani / Kijambiani / Kitumbatu-Gomani / Kikibeni / Kinungwi]
SM1sg-do-PstF
- c. N-tend-e. [Kijambiani / Kipaje]
SM1sg-do-PstF

(8) 'She/He wrote a letter.'

- a. A-li-andik-a barua. [Kiswahili Sanifu / Kiunguja-Mjini]
SM3sg-Pst-write-FV cl9-letter
- b. Ka-andik-i (> kandiki) baruwa. [Kichaani / Kijambiani / Kitumbatu-Gomani / Kikibeni / Kinungwi /
SM3sg-write-PstF cl9-letter Kipaje]

(9) 'You saw her/him.'

- a. U-li-mw-on-a. [Kiswahili Sanifu / Kiunguja-Mjini]
SM2sg-Pst-OM3sg-see-FV
- b. Ku-m-on-o. [Kichaani / Kitumbatu-Gomani / Kikibeni / Kinungwi / Kijambiani / Kipaje]
SM2sg-OM3sg-see-PstF

(10) 'We pulled the rope.'

- a. Tu-li-vut-a kamba. [Kiswahili Sanifu / Kiunguja-Mjini]
SM1pl-Pst-pull-FV cl9-rope
- b. Tu-vut-u kamba. [Kichaani / Kitumbatu-Gomani / Kikibeni / Kinungwi / Kijambiani /
SM1pl-pull-PstV cl9-rope Kipaje]

Sentensi za kukanusha zenye njeo iliyopita zinaonyeshwa katika mifano kuanzia (11) mpaka (15): Mifano ya (11)a mpaka (15)a ni ya sentensi za Kiswahili Sanifu na Kiunguja-Mjini, mifano ya (11)b mpaka (15)b ni ya sentensi za Kichaani, Kitumbatu-Gomani, Kikibeni, Kinungwi, halafu mifano ya (11)c mpaka (15)c ni ya sentensi za Kijambiani na Kipaje. Mifano hii inatuonyesha kwamba katika Kiswahili Sanifu na Kiunguja-Mjini kiambishi-njeo cha kukanusha cha njeo iliyopita ni *-ku-*, lakini katika lahaja nyingine isipokuwa Kijambiani na Kipaje kiambishi hicho ni *-e-*. Na kama tunavyoona katika mfano wa (15)b, kunatokea mabadiliko ya sauti kwenye vokali ya kiambishi-kiini cha kukanusha kwa ajili ya taathira ya kiambishi-njeo cha kukanusha cha njeo iliyopita *-e-*.

Na katika Kijambiani na Kipaje, kiambishi-njeo cha kukanusha cha njeo iliyopita ni *-li-* kama tunavyoona katika mifano ya (11)c mpaka (15)c. Jambo hili pia linatuvutia kwa sababu kiambishi-njeo hiki kinatumika kwa

sentensi yakinishi za njeo iliyopita katika Kiswahili Sanifu na Kiunguja-Mjini. Isitoshe, kama inavyoonyeshwa katika mifano ya (6)b mpaka (10)b na (6)c na (7) c, kunatokea kunakili vokali ya mzizi wa kitenzi katika muundo wa uyaikinishi wa njeo iliyopita, lakini kunakili huko hakutokei katika muundo wa kukanusha, vokali wa mwisho ni -a.

(11) ‘I didn’t cut meat.’

- a. Si-ku-kat-a nyama. [Kiswahili Sanifu / Kiunguja-Mjini]
 NegSM1sg-NegPst-cut-FV cl9-meat
- b. Si-e-kat-a (> Sekata) nyama. [Kichaani / Kitumbatu-Gomani / Kikibeni / Kinungwi]
 NegSM1sg-NegPst-cut-FV cl9-meat
- c. Si-li-kat-a nyama. [Kijambiani / Kipaje]
 NegSM1sg-Pst-cut-FV cl9-meat

(12) ‘I didn’t do.’

- a. Si-ku-fany-a. [Kiswahili Sanifu / Kiunguja-Mjini]
 NegSM1sg-NegPst-do-FV
- b. Si-e-tend-a (> Setenda). [Kichaani / Kitumbatu-Gomani / Kikibeni / Kinungwi]
 NegSM1sg-NegPst-do-FV
- c. Si-li-tend-a. [Kijambiani / Kipaje]
 NegSM1sg-Pst-do-FV

(13) ‘She/He didn’t write a letter.’

- a. Ha-ku-andik-a barua. [Kiswahili Sanifu / Kiunguja-Mjini]
 NegSM3sg-NegPst-write-FV cl9-letter
- b. Ha-e-kwandik-a (> Hekwandika) baruwa. [Kichaani / Kitumbatu-Gomani / Kikibeni / Kinungwi]
 NegSM3sg-NegPst-write-FV cl9-letter
- c. Ha-li-kwandik-a baruwa. [Kijambiani / Kipaje]
 NegSM3sg-Pst-write-FV cl9-letter

(14) ‘You didn’t see her/him.’

- a. Hu-ku-mw-on-a. [Kiswahili Sanifu / Kiunguja-Mjini]
 NegSM2sg-NegPst-OM3sg-see-FV
- b. Hu-e-m-on-a (> Hwemona). [Kichaani / Kitumbatu-Gomani / Kikibeni / Kinungwi]
 NegSM2sg-NegPst-OM3sg-see-FV
- c. Hu-li-mw-on-a. [Kijambiani / Kipaje]
 NegSM2sg-Pst-OM3sg-see-F

(15) ‘We didn’t pull the rope.’

- a. Hatu-ku-vut-a kamba. [Kiswahili Sanifu / Kiunguja-Mjini]
 NegSM1pl-NegPst-pull-FV cl9-rope
- b. Hatu-e-vut-a (> Hetwevuta) kamba. [Kichaani / Kitumbatu-Gomani / Kikibeni / Kinungwi]
 NegSM1pl-NegPst-pull-FV cl9-rope
- c. Hatu-li-vut-a kamba. [Kijambiani / Kipaje]
 NegSM1pl-Pst-pull-FV cl9-rope

Na lazima tutaje kwamba katika kauli ya kutendwa ya njeo iliyopita hakutokei kunakili vokali ya mzizi wa kitenzi kama inavyoonyeshwa katika mifano (16)b na (16)c.

(16) ‘Ali was hit by Juma.’

- a. Ali a-li-pig-w-a na Juma. [Kiswahili Sanifu / Kiunguja-Mjini]
 Ali SM3sg-Pst-hit-Pass-FV by Juma
- b. Ali ka-pig-w-a ni Juma. [Kichaani / Kikibeni / Kinungwi / Kijambiani / Kipaje]
 Ali SM3sg-hit-Pass-FV by Juma
- c. Ali ka-but-w-a ni Juma. [Kitumbatu-Gomani]
 Ali SM3sg-hit-Pass-FV by Juma

Sasa tutazame njeo ya hali timilifu. Mfano wa (17)a ni wa sentensi za Kiswahili Sanifu na Kiunguja-Mjini, (17)b ni sentensi za Kichaani, Kitumbatu-Gomani, Kijambiani, Kikibeni, na Kinungwi, na (17)c ni Kitumbatu-Gomani, Kikibeni na Kinungwi. Kama tunavyoona katika mfano wa (17)a na (17)b, kuna utofauti wa kiambishi-njeo cha hali timilifu, kwa mfano katika Kiswahili Sanifu ni *-me-*, kilichotokana na kitenzi *-mala* au *-maliza* (‘finish’), lakini kisarufi hakuna tofauti baina ya lahaja na lahaja. Na isitoshe, mfano wa (17)c unaonyesha kuwa kiambishi-njeo cha njeo iliyopita kinatumiwa katika Kitumbatu-Gomani, Kikibeni, Kinungwi hasa kwa wasemaji wazee, wasemaji vijana wanatumia zaidi muundo wa (17)b. Kama tunavyoona katika mfano wa (17)d, katika Kijambiani na Kipaje pia kiambishi-njeo cha hali timilifu hakitumiwi sana, badala yake kiambishi-njeo cha njeo iliyopita kinatumika. Zaidi ya hayo, katika Kichaani baadhi ya watu wanasema kama sentensi iliyoko chini ya mfano namba (17)d. Bado hatujafafanua vizuri lakini inawezekana kusema kwamba viambishi-njeo viwili vinatumika kabla ya kitenzi, kwani katika sentensi hiyo kama tunavyoona kiambishi-njeo cha hali timilifu *-ma-* na kiambishi cha njeo iliyopo *-na-* vinatumika kwa pamoja.

(17) ‘I have seen her/him.’

- a. Ni-me-mw-on-a. [Kiswahili Sanifu / Kiunguja-Mjini]
 SM1sg-Perf-OM3sg-see-FV
- b. Ni-ma-m-on-a. [Kichaani / Kitumbatu-Gomani / Kikibeni / Kinungwi]
 SM1sg-Perf-OM3sg-see-FV
- c. Ni-m-on-o. [Kitumbatu-Gomani / Kikibeni / Kinungwi]
 SM1sg-OM3sg-see-PstV
- d. M-m-on-o. [Kijambiani / Kipaje]
 SM1sg-OM3sg-see-PstV
- cf. Yembe zi-ma-na-az-a uz-w-a. [Kichaani]
 cl10.mango SM10-Perf-Pres-start-FV sell-Pass-FV
 ‘Mangos have been already started being for sale.’

Na kama tunavyoona katika mfano wa (18), muundo wa kutumia kitenzi *-isha* pia unatumika kwa kumaanisha hali timilifu kabisa katika lahaja hizi.

kuna mfano wa sentensi inayotumia kopyula yenye kiambishi-njeo cha njeo iliyopita kama *nalikuwa*, sawasawa na mfano wa Kikibeni unaonyeshwa hapa. Muundo huu unaonekana pia katika ‘Kiswahili cha Kale’ (Old Swahili). Imehakikishwa kwamba kiambishi-njeo *-ali-* kinatumika si pamoja na kopyula tu bali pamoja na vitenzi vya kawaida pia kutokana na sentensi zilizomo katika *Hekaya za Abunuwas*. Lakini Kikibeni kinatumia muundo mmoja wa (21)d na (22)d unaotumika katika Kichaani vilevile, na muundo huu ndio unaotumiwa zaidi siku hizi isipokuwa kwa wasemaji wazee.

Jambo jingine linalotusisimua ni kwamba kama inavyoonyesha mifano ya (21)c, (22)c, (21)d na (22)d Kitumbatu-Gomani na Kinungwi yaani lahaja za sehemu za Kaskazini na Kijambiani yaani lahaja ya sehemu ya Kusini zina muundo unaofanana sana. Na tena, lazima tuziangalie lahaja za Kitumbatu-Gomani na Kichaani pia. Kwa mujibu wa maelezo ya wanakijiji wa Chaani wengi wao wametoka Kisiwa cha Tumbatu na kuhamia Chaani na vijiji vingine vilivyoko karibu na Chaani. Na wanajiona wanasema ‘Kitumbatu’. Lakini kutokana na data tunazoonza sasa inadhihirika kwamba ingawa muundo wa (21)c na (21)d ama muundo wa (22)c na (22)d unafanana sana kama vile hakuna kiambishi-njeo cha njeo iliyopita, lakini kuna tofauti kidogo kama kopyula ya njeo iliyopita ni *-vu* au *-evu*. Hayo yanatambua kuwa lazima tuendelee na utafiti wetu kwa undani zaidi ili kufafanua na kufahamu vizuri utofauti wa lahaja za Kiswahili.

(20) ‘I am a student.’

a. Mimi ni mw-anafunzi. [Kiswahili Sanifu / Kiunguja-Mjini]

Pron1sg Cop cl1-student

b. Miye mwanafuzi. [Kichaani / Kitumbatu-Gomani / Kikibeni / Kinungwi / Kipaje]

Pron1sg cl1-student

c. Mie ni-wa mwanafunzi. [Kijambiani]

Pron1sg SM1sg-be-FV cl1-student

(21) ‘I was a student.’

a. Ni-li-kuw-a mw-anafunzi. [Kiswahili Sanifu / Kiunguja-Mjini]

SM1sg-Pst-be-FV cl1-student

b. Ni-ali-kuw-a (> nyalikuwa) mw-anafuzi. [Kikibeni]

SM1sg-Pst-be-FV cl1-student

c. Ni-vu mw-anafuzi. [Kitumbatu-Gomani / Kinungwi]

SM1sg-be. Pst cl1-student

d. Ni-evu mw-anafuzi. [Kichaani / Kikibeni / Kijambiani / Kipaje]

SM1sg-be. Pst cl1-student

(22) ‘You had a cow.’

a. U-li-kuw-a na ng’ombe. [Kiswahili Sanifu / Kiunguja-Mjini]

SM2sg-Pst-be-FV with cl9-cow

b. Ku-ali-kuw-a (> Kwalikuwa) na ng’ombe. [Kikibeni]

SM2sg-Pst-be-FV with cl9-cow

c. Ku-vu na ng’ombe. [Kitumbatu-Gomani / Kinungwi]

SM2sg-be. Pst with cl9-cow

d. Ku-evu (> Kwevu) na ng'ombe. [Kichaani / Kikibeni / Kijambiani / Kipaje]
 SM2sg-be. Pst with cl9-cow

2.3. Kauli Zinazotumia Viambishi-Rejeshi

Katika sehemu hii tunaangalia tofauti za kimuundo za kauli zinazotumia viambishi-rejeshi: mfano wa (23)a ni kauli ya Kiswahili Sanifu na Kiunguja-Mjini, (23)b ni Kichaani, Kikibeni, na Kinungwi, (23)c na (23)d ni Kitumbatu-Gomani, na (23)e na (23)f ni Kijambiani na Kipaje. Kama mfano wa (23)b unavyoonyesha, katika Kichaani, Kikibeni, na Kinungwi, kiambishi-njeo cha njeo iliyopita hakitokei katika kauli zinazotumia viambishi-rejeshi. Kwa Kitumbatu-Gomani, ambacho kinasemwa karibu na kijiji cha Chaani kijiografia, kitenzi 'give' ni tofauti na cha Kichaani kama tunavyoona katika mfano wa (23)c. Isitoshe, kitenzi hiki kinatumika katika Kijambiani na Kipaje lahaja zinazosemwa katika sehemu za Kusini. Kitumbatu-Gomani kina muundo mwingine wa ?kauli zenye viambishi-rejeshi kama katika mfano wa (23)d. Muundo huo vilevile unafanana sana na ule wa (23)e yaani muundo unaotumika katika Kijambiani na Kipaje. Lakini, wasemaji vijana wa Kitumbatu-Gomani hawatumii sana muundo wa (23)d badala yake wanatumia (23)c, hata wasemaji wa Kijambiani na Kipaje pia vijana hawatumii sana muundo wa (23)e zaidi inaonekana wanatumia ule wa (23)f. Yaani inawezekana kusema kuwa muundo wa (23)d na (23)e ni wa kizamani.

(23) 'the person who gave me a book'

a. m-tu	a-li-ye-ni-p-a	ki-tabu	[Kiswahili Sanifu / Kiunguja-Mjini]
cl1-person	SM3sg-Pst-Rel1-OM1sg-give-FV	cl7-book	
b. m-tu	a-ye-ni-p-a	buku	[Kichaani / Kikibeni / Kinungwi]
cl1-person	SM3sg-Rel1-OM1sg-give-FV	cl5-book	
c. m-tu	a-ye-ni-k-a	ki-tabu	[Kitumbatu-Gomani]
cl1-person	SM3sg-Rel1-OM1sg-give-FV	cl7-book	
d. m-tu	mw-e-ni-k-a	ki-tabu	[Kitumbatu-Gomani]
cl1-person	RelSM.cl1-Pst-OM1sg-give-FV	cl7-book	
e. m-tu	mw-a-n-k-a	ki-tabu	[Kijambiani / Kipaje]
cl1-person	RelSM.cl1-Pst-OM1sg-give-FV	cl7-book	
f. m-tu	a-li-ye-n-k-a	ki-tabu	[Kijambiani / Kipaje]
cl1-person	SM3sg-Pst-Rel1-OM1sg-give-FV	cl7-book	

2.4. Dhamira Amri

Mwishoni tuangalie mifano ya dhamira amri. Mfano wa (24) ni wa muundo wa dhamira amri yenye kiambishi-yambwa cha mtu mmoja: (24)a ni muundo wa Kiswahili Sanifu na Kiunguja-Mjini, (24)b ni wa Kichaani, Kitumbatu-Gomani, Kikibeni, (24)c ni wa Kijambiani na Kipaje, na (24)d ni wa Kinungwi. Kama tunavyoona, ikiwa kiambishi-yambwa kina maana ya 'mtu mmoja', kama katika (24)b, (24)c na (24)d vokali ya kiishio itakuwa vokali ya msingi yaani -a. Lakini kama mfano wa (25) unavyoonyesha, ikiwa kiambishi-yambwa kina maana ya 'watu wawili au zaidi', vokali ya kiishio itakuwa vokali ya dhamira matilaba yaani -e.

(24) ‘Make bread for me.’

- | | | |
|----------------------|-----------|--|
| a. Ni-tengenez-e-e | mi-kate. | [Kiswahili Sanifu/ Kiunguja-Mjini] |
| OM1sg-make-Appl-SBJF | cl4-bread | |
| b. Ni-tend-e-ya | mi-kate. | [Kichaani / Kitumbatu-Gomani / Kikibeni] |
| OM1sg-make-Appl-FV | cl4-bread | |
| c. N-tend-e-ya | mi-kate. | [Kijambiani / Kipaje] |
| OM1sg-make-Appl-FV | cl4-bread | |
| d. Ni-yund-i-ya | mi-kate. | [Kinungwi] |
| OM1sg-make-Appl-FV | cl4-bread | |

(25) ‘Make bread for us.’

- | | | |
|----------------------|-----------|---|
| a. Tu-tengenez-e-e | mi-kate. | [Kiswahili Sanifu/ Kiunguja-Mjini] |
| OM1pl-make-Appl-SBJF | cl4-bread | |
| b. Tu-tend-e-le | mi-kate. | [Kichaani / Kijambiani / Kitumbatu-Gomani / Kikibeni] |
| OM1pl-make-Appl-SBJF | cl4-bread | |
| c. Tu-tend-e-e | mi-kate. | [Kijambiani / Kipaje] |
| OM1pl-make-Appl-SBJF | cl4-bread | |
| d. Tu-yund-i-le | mi-kate. | [Kinungwi] |
| OM1pl-make-Appl-SBJF | cl4-bread | |

3. Hitimisho

Katika makala hii tumeangalia utofauti kadhaa wa kimsamiati na kisarufi wa lahaja za Kiswahili kisiwani Unguja. Tumbaini kwamba zipo tofauti zisizo ndogo wala tusizoweza kuzipuuzia si baina ya lahaja nyingine za Kiswahili na Kiswahili Sanifu / Kiunguja-Mjini tu, bali pia baina ya lahaja na lahaja.

Kwanza, tumetaja kwamba Kitumbatu-Gomani inayotajwa kuwa ni lahaja ya sehemu ya Kaskazini na Kijambiani inayotajwa kuwa ni lahaja ya sehemu ya Kusini kwa mujibu wa tafiti zilizofanyika zamani, ingawa kijiografia ziko mbali sana lakini lahaja hizo zinafanana miundo yao kama muundo wa sentensi zenye kiambishi-njeo cha njeo iliyopita na muundo wa sentensi za njeo iliyopita zinazotumia kopyula. Na upande mwingine, Kichaani na Kikibeni, yaani lahaja zinazosemwa katika vijiji vilivyoko karibu karibu na zinazosemekana ni lahaja za Kaskazini, zina tofauti za kimuundo kama muundo wa sentensi za njeo iliyopita zinazotumia kopyula.

Pili, kutokana na data tulizoon, upo utofauti kati ya lahaja na lahaja. Utofauti huu unategemeana na tofauti za kijiografia na za kielimu pia. Kwa mfano, kama data za Kijambiani zinavyoonyesha, kuna “lahaja ya Kijambiani kwa wazee” na “lahaja ya Kijambiani kwa vijana”, yaani tuseme kuna “vilahaja” katika lahaja moja, na wasemaji wanachagua na kubadilisha kilahaja fulani ili wasikilizaji wafahamu vizuri³⁾.

³⁾ Uchaguzi wa kutumia lahaja au kilahaja unatokea katika muktadha mwingine: kwa mfano lahaja au kilahaja fulani kinachaguliwa kwa sababu msemaji na msikilizaji wanakaa katika vijiji vilivyoko karibu yaani wote wawili wanafahamiana/wanaelewana kwa kutumia lahaja au kilahaja hicho, ama, lahaja au kilahaja fulani kinaweza kutumiwa na msikilizaji anayekaa mbali kijiografia. Kwa maneno mengine, msemaji anatumia “lahaja au kilahaja tofauti” kwa kulingana

Tatu, kiambishi-njeo cha hali timilifu kinaonyesha utofauti baina lahaja ingawa kinatokana na kitenzi kimoja. Jambo hili linatuambia kuwa kuna utofauti wa njia na viwango vya kubadili umbo la viambishi vya kisarufi na usanifu, na kila lahaja ina hali na kiwango tofauti cha kuhifadhi muundo wa kizamani, kubadilisha umbo la viambishi n.k.

Na tena, hili linaonekana si kisiwani Unguja tu bali pia Tanzania bara au zaidi katika maeneo yanayozungumzwa lugha za Kibantu. Kwa mfano kopyula ya njeo iliyopita *-evu* na kiambishi-njeo cha njeo iliyopita *-ali-* kinaonekana si nchini Tanzania tu bali pia katika sehemu nyingine zinapozungumzwa lugha nyingine za Kibantu. Kiambishi-njeo *-ali-* kimetambulikana kuwa cha ‘Kiswahili cha Kale’, na kimeingia katika lahaja kadhaa za kisiwani Unguja, kwa hivyo inawezekana kuwa kuna uhusiano fulani baina ya ‘Kiswahili cha Kale’ na lahaja hizi za kisiwani Unguja. Kufanya utafiti juu ya lahaja za kisiwani Unguja kunaweza kutufungulia milango ya kufahamu mkondo/mwenendo/mwelekeo wa kubadilika au kurahisika kutoka ‘Kiswahili cha Kale’ kwenda lahaja za sehemu za Kaskazini au za Kusini au Kiswahili Sanifu. Na kadhalika, kusoma hali mbalimbali za kiisimu zinazonekana katika Kiswahili na lugha nyingine za Kibantu kutatusaidia pia kufahamu vizuri zaidi mwenendo wa kusanifika kwa lugha fulani na kutatuongoza ili tupate ufafanuzi mpya wa mabadiliko na maendeleo ya kimofosintaksia katika lugha za Kibantu.

Makala yetu hii inasema kuwa kunahitajika kuvuka mipaka ya kufanya utafiti wa kizamani na wa kijiografia na kuchukua hatua ya kwenda kufanya utafiti wa kina kirefu zaidi na unaoangalia hali nzima kwa kutumia mbinu zote za kitafiti (qualitative and quantitative) ili kufafanua kikamilifu utofauti wa lahaja za kisiwani Unguja. Siku za mbeleni tunaweza kufanya utafiti wa kulinganisha kwa dhati hali fulani fulani za kiisimu za lahaja za kisiwani Unguja zinazoweza kutupa dokezo/njia za kufafanua hali za kiisimu za ‘Kiswahili cha Kale’ na lugha nyingine za Kibantu na kuangalia kwa mitazamo yote miwili ya utafiti wa kiisimu yaani kisinkronia na kidaikronia. Na wakati mmoja, inahitajika pia kufanya utafiti wa kuchunguza mabadiliko yoyote ya lahaja yanayoweza kutokea kutokana na ?kuwasiliana/kuingiliana na Kiswahili Sanifu.

Pamoja na utafiti elezi, lazima tufanye utafiti wa kukusanya data za kiisimu-jamii juu ya matumizi ya lugha na hali au hadhi ya kijamii ya lahaja zenyewe. Utafiti huu utatusaidia kufahamu kuwa ni hali zipi za kiisimu-jamii zinazoweza kuhusishwa na mienendo ya ‘Kiswahili’ hivyo.

Shukrani

Makala hii isingekamilika bila ya misaada ya wahojiwa wangu mimi Keiko na wahojiwa wake Kumiko pia. Sisi sote tulisaidiwa sana huko kisiwani Unguja kila tulipofanya utafiti wetu. Kwa sasa hatuwezi kutaja majina yao mmoja mmoja lakini kwa dhati yetu tunawashukuru kwelikweli. Mbali na wahojiwa hao, kila wakati tulisaidiwa sana na wanakijiji ili tuendeleo na utafiti wetu vizuri kama kutupa chakula, kututayarishia mahali pa kulala, n.k. Tunawashukuru mno.

Halafu lazima tutaje jina lake Mwl. Zainabu kwa msaada wake mkubwa. Ametupitia na kuturekebisha makala hii kama kawaida. Tunamshukuru sana sana.

na msikilizaji wake. Uchaguzi wa lahaja au kilahaja wa aina hii unaonekana si baina ya lahaja na lahaja tu bali baina ya lahaja na Kiswahili Sanifu pia.

Mwishoni tuongeze kutaja kwamba ikiwa kuna makosa ama kasoro ya maandiko ya makala hii, bila shaka ni wajibu wetu, na si wajibu wao wahojiwa na wasaidizi wetu.

Vifupisho

-	mpaka wa mofimu
1sg, 1pl	nafsi ya kwanza-umoja, nafsi ya kwanza-wingi
2sg, 2pl	nafsi ya pili-umoja, nafsi ya pili-wingi
3sg, 3pl	nafsi ya tatu-umoja, nafsi ya tatu-wingi
Appl	kiambishi-nyambulishi cha kutendea
BF	kiishio cha msingi
Cop	kopyula
Fut	njeo ijayo
FV	vokali ya mwisho
Inf	kiambishi cha -ku- ya kitenzi kisoukomo
Neg	kiambishi-ukanushi
NegF	kiishio cha ukanushi cha njeo iliyopo
OM	kiambishi-yambwa
Pass	kiambishi-nyambulishi cha kutendwa
Perf	hali timilifu / hali timilifu kabisa
Pron	kiwakilishi
Prs	njeo iliyopo
Pst	njeo iliyopita
PstF	kiishio cha njeo iliyopita
Rel	kiambishi-rejeshi
SBJF	kiishio cha dhamira matiraba
SM	kiambishi-kiima

Marejeo

- Bryan, M. A. 1959. "Swahili Group". *The Bantu Languages of Africa*. pp.126-129. Oxford University Press.
- Miyazaki, Kumiko. 2014. "Repoti juu ya Kijambiani (2) - Maelezo ya Kisarufi ya Kijambiani -". *Swahili & African Studies* No. 25. pp.145-161. (kwa Kijapani)
- Nurse, D. & T. J. Hinnebusch. 1993. *Swahili and Sabaki: A Linguistic History*. University of California Press.
- Takemura, Keiko. 2018. "Nini ndiyo 'Lugha' - Kuzingatia Tofauti baina ya 'Lahaja' na 'Kiswahili Sanifu' Visiwani Zanzibar -". *Swahili & African Studies* No.29. pp.167-187.
- . 2017. "Miundo ya Sentensi za Njeo Iliyopita katika Kitumbatu-Gomani - Kwa Kulinganisha na Kichaani na Kiswahili Sanifu -". *Swahili & African Studies* No.28. pp.109-121.

- . 2016. “Miundo ya Sentensi zenye Kitenzi ‘-wa’ katika Kichaani - Kulinganisha na Kiswahili Sanifu -”. *Swahili & African Studies* No.27 pp.53-63.
- Whitely, W.H. 1956. *Ki-mtang’ata: A Dialect of the Mrima Coast - Tanganyika*. East African Swahili Committee, Makerere College, Kampala.
1935. *Hekaya za Abnuwas na Hadithi Nyingine*. The Macmillan Press Ltd.